

Thubutu Kuwa MKARIMU!

Ninaangaza nuru yangu kwa kuwa mkarimu kwa wengine.

Halo!

Mimi ni Claudia na Ninaishi Australia.

Kaka wa Claudia, Tyler

Ninasimama imara kwa ajili ya Wengine

Mvulana katika darasa langu shuleni anapata wakati mgumu kujifunza. Najitokeza kwa ajili yake wakati watu wanapomchokoza, na ninamsaidia darasani wakati anapohitaji msaada. Mwalimu wangu alisema huu ni mwaka pekee mvulana huyu anajiona kuwa naye ni sehemu ya darasa lake.



Mwanasesere Dubu Mdogo

Wakati mjomba wa mwalimu wangu alipofariki, alikuwa na huzuni sana. Hajui kuhusu Kanisa, kwa hivyo Nilimwambia kuwa Baba wa Mbinguni anampenda. Nilimtengezeza kadi na kumwambia kwamba atamuona mjomba wake tena. Nilimpa mwanasesere dubu wangu mdogo maalumu ili kumsaidia katika nyakati za huzuni.



Marafiki wenye Bahati

Jirani yangu Olivia anapata taabu ya kutembea, kuongea, na kusikia. Mama yake Olivia husema kwamba Olivia ana bahati kuwa na rafiki kama mimi. Mimi nina bahati pia!



Kuimba na Roho Mtakatifu

Ninapenda kuimba nyimbo kutoka kwenye *Kitabu cha Nyimbo za Watoto*. Familia yangu husema huwasaidia wao kuhisi Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hunipa hisia nzuri za ndani.



JE, NI KWA JINSI GANI WEWE UNaweza KUANGAZA?

THUBUTU kufanya urafiki na mtu ambaye hana marafiki wengi.
THUBUTU kumsaidia jirani yako.
THUBUTU kumwalika rafiki kanisani.
THUBUTU kuimba!



TUTUMIE NYOTA!

Je, ni kwa jinsi gani unafanya nuru yako iangaze, kama Yesu alivyo-tuomba kufanya? Tuma kwa barua pepe picha ya nyota yako ikiwa na hadithi yako na picha yako, pamoja na ruhusa ya wazazi wako kwenda liahona@ldschurch.org.